THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**121/1** **KISWAHILI I**

*(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)*

*Muda: Saa 3* *2009 Februari, 12 Alhamisi Asubuhi*

---

*MAELEKEZO*

1. Karatasi hii ina maswali **13** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Maswali **yote** yana alama sawa.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## HISTORIA

1. "Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu J.K. Nyerere ametoa mchango mkubwa katika kukikuza na kukieneza Kiswahili nchini Tanzania". Thibitisha kauli hiyo kwa kutoa mifano bayana.

2. Kwa kutumia ushahidi wa kiisimu **au** kihistoria jadili kuhusu mganganyiko unaosababishwa na nadharia tete katika kuelezea chimbuko la Kiswahili.

3. Mkutano wa kwanza wa Kamati ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki uliofanyika Januari 1930 uliazimia nini? Eleza maazimio hayo.

## SEHEMU B (alama 20)

## SARUFI

4. Kwa kutoa mifano, onesha maumbo mbalimbali ya kitenzi kishirikishi (t).

5. "Neno linaweza kuwa nomino, kielezi au kitenzi kutokana na jinsi linavyotumiwa". Thibitisha kauli hii kwa kuyatumia maneno yafuatayo katika sentensi:

   (a) Panda.
   (b) Kaa.

6. Taja kazi **tano (5)** za mofimu "Ki" na kwa kila kazi itungie sentensi moja.

## SEHEMU C (alama 20)

## MATUMIZI

7. Eleza faida za tamathali za semi katika lugha.

8. "Matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania yamekifanya kikue licha ya baadhi ya watu kukipiga vita". Jadili kauli hii kwa kutoa mifano.

9. Fafanua makosa ya kisarufi yanayosababishwa na watumiaji wa Kiswahili.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

**mrama**, kama vile chumba hicho kilikuwa kikielea juu ya mawimbi yenye kusukasuka. Bahati alishika hodari **kingo** za kitanda chake asiporomoke na kuanguka. Kichwani mlikuwa na mgongano wa vipande vya mawazo, kwa sababu ya vituko vya jana.

Alikumbuka kama alilala na viatu, akapeleka mkono taratibu akavivua. Alijaribu kusimama, hali akiangaza macho chumbani na kujaribu kutuliza fikra zake. Ngozi ya mwili ilikuwa kavu, na viungo vikamkaza, hata mwili wote ukamwuma. Alijinyosha mfano wa nyoka, akaenda mwayo na kupepesukia dirishani, akalifungua na kuchungulia nje.

Kila alichotazama kule nje kilikuwa kimefunikwa na **ukungu**---.

Maswali:

(a) Unadhani ni kwa nini kila kitu kilikuwa kimefunikwa kwa ukungu?

(b) Mwandishi anamaanisha nini anaposema "--- usingizi ukamwonea huruma ukamchukua hima na kumpumzisha kitandani ---".

(c) Unafikiri ni kwa nini Bahati alilia kwa majuto, mapenzi na upweke?

(d) Mwandishi ana maana gani anaposema, "Ndiye mkosaji na ndiye sababu".

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari uliyoisoma.

(i) Kifudifudi.
(ii) Simanzi.
(iii) Kite.
(iv) Mayowe.
(v) Mrama.
(vi) Kingo.
(vii) Ukungu.
(viii) Usumba.

(f) Fupisha habari hii kwa maneno yasiyopungua **mia moja na arobaini (140)** na yasiyozidi **mia moja na hamsini (150)**.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 20)

### UTUNGAJI

10. Andika risala yenye maneno yasiyozidi **mia nne (400)** na yasiyopungua **mia tatu (300)** ambayo itasomwa katika tafrija ya kumuaga Mkuu wenu wa shule ambaye amepewa wadhifa mwingine.

11. Andika insha ya maneno yasiyozidi **mia nne (400)** na yasiyopungua **mia tatu (300)** juu ya maisha ya uanafunzi.

12. Shirika la Elimu Tanzania limefungua matawi yake katika kila wilaya hapa nchini. Andika barua katika gazeti la "Mtanzania" kuwafahamisha wanafunzi wenzako kuhusu huduma mbalimbali wanazoweza kuzipata katika shirika hilo hapo wilayani kwao. Jina lako ni Haki Elimu, Shule ya Sekondari Kasimpya, S.L.P. 1957, Kipatimu, Kilwa.

## SEHEMU E (alama 20)

### UFAHAMU

13. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:

Bahati alikuwa amelala **kifudifudi** kitandani pake, akilia kwa kwikwi. Akilia majuto, mapenzi na upweke; akilila ndoto zake. Mara alijiona yuko peke yake katika dunia. Ile kamba ya tumaini iliyokuwa akiining'inia aliona imemponyoka akawa hana cha kushika. Alijiona mgeni hali yuko kwao, tena kitandani pake.

Alisikitika akaona amekimbiwa na mwenyeji wake wa uhai. Sasa hakuthamini kitu chochote kingine ila Iddi; ambaye alikwisha mpoteza. Hakuwa na mwingine, wala hangemtaka mwingine; nani angekuwa kama Iddi? Haya ndiyo mawazo aliyokuwa akipigana nayo.

Ah! Lakini aliona yote hayo aliyataka mwenyewe. Yeye ndiye aliyemfukuza, ndiye mkosaji na ndiyo sababu. Vile alivyofanya sivyo, kabisa sivyo, kwani ----. Lawama zake zilikuwa bure maana yeye ndiye wa kulaumiwa. Alijuta kutumia nguvu, bora angetumia upole wa siasa au angekubali kushiriki jambo aliloambiwa na Iddi. Bora ubaya wa nia ya Iddi kuliko hali aliyokuwa nayo sasa. Kwa nini asikubali, kwa nini?

Bahati alilia **kite** na **simanzi**, hata usingizi ukamwonea huruma; ukamchukua hima na kumpumzisha kitandani. Alizindushwa na vishindo vya mwenda msikitini, maana tayari kulikwishapambazuka. Saa ya Bahati siku zote ilikuwa wapita njia. Alikuwa amekwishazoea kukisia wakati wa nyendo za wale waendao kazini, shule, msikitini, ndege za abiria na waadhini.

Punde hivi, alijizoazoa juu ya kitanda cha **mayowe**, chenye godoro la **usumba**, akaketi ukingoni. Macho yalikuwa yameiva na kuvimba, kichwa kikawa kizito, mfano wa mtu aliyekesha. Aliona sakafu ya chumba chake ikienda



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org